**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

# MWONGOZO WA ZIARA YA NYUMBANI KWA WANAFUNZI WENYE MAHITAJI MAALUMU

**JUNI, 2023**

**© Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, 2023**

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa, kurudufu wala kufasili au kutoa Mwongozo huu kwa namna yoyote ile bila idhini ya Kamishna wa Elimu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

ISBN…….

Toleo la Kwanza, 2023

Umechapishwa na:

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,

Mji wa Serikali,

Eneo la Mtumba,

Mtaa wa Afya,

S.L.P 10,

**40479 DODOMA, TANZANIA**

# YALIYOMO


**ORODHA YA VIFUPISHO.............................................v**

**SHUKRANI.........................................................vi**

**DIBAJI...............................................................vii**

**SURA YA KWANZA...................................................1**

UTANGULIZI...........................................................1

1.0 Usuli.................................................................1

1.1. Muundo wa Mwongozo.......................................4

1.2 Walengwa wa Mwongozo....................................4

1.2.1 Lengo kuu la Mwongozo wa Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum...............4

1.2.2 Malengo Mahususi ya Mwongozo wa Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum..........................................................5

1.3 Wanufaika wa Mwongozo.....................................5

1.4 Watumiaji wa Mwongozo......................................6

1.5 Matokeo Tarajiwa ya Ziara za Nyumbani..............6

1.6 Matokeo Tarajiwa ya Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum.......................7

**SURA YA PILI........................................................ 8**

DHANA YA ZIARA ZA NYUMBANI................................ 8

2.0 Maana ya Ziara za Nyumbani...............................8

2.1 Umuhimu wa Ziara za Nyumbani......................... 8

2.2 Mambo ya Kuzingatia Kabla ya Ziara..................8

2.3 Mambo ya Kuzingatia Wakati wa Ziara................ 9

2.4 Mambo ya Kuzingatia Baada ya Ziara................10

**SURA YA TATU..........................................................11**

MAJUKUMU MBALIMBALI YA WADAU KATIKA ZIARA ZA NYUMBANI..................................................11

3.0 Wadau wa Elimu wana majukumu yafuatayo......11

3.1 Majukumu ya Watumiaji wa Mwongozo..............11

3.1.1 Majukumu ya Mwalimu Anayefundisha Mwanafunzi Mwenye Mahitaji Maalumu..............11

3.1.2 Majukumu ya Mwalimu Mkuu..............................12

3.1.3 Majukumu ya Afisa Elimu Kata........................... 12

3.1.4 Majukumu ya Afisa Elimu Maalumu...................12

3.1.5 Majukumu ya Afisa Elimu Msingi........................13

3.1.6 Majukumu Mthibiti Ubora wa Shule wa Wilaya.. 13

3.1.7 Viongozi wa Serikali za Mtaa/Kijiji......................14

**SURA YA NNE..........................................................15**

UFUATILIAJI NA TATHMINI..........................................15

4.0. Utangulizi..........................................................15

4.1 Maana...............................................................15

4.2 Mbinu za Ufuatiliaji na Tathimini za Ziara a Nyumbani.........................................................16

**REJEA.................................................................17**

# ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| BEST | Basic Education Statistics in Tanzania |
| MoEST | Ministry of Education, Science and Technology |
| OR-TAMISEMI | Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| UWAWA | Umoja wa Walimu na Wazazi |
| WyEST | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia |

# SHUKRANI

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatoa shukrani za dhati kwa wadau wote walioshiriki katika uandaaji wa mwongozo huu. Kipekee, Wizara inatoa shukrani kwa Wakuu wa Shule za Msingi na Sekondari wa Serikali na wasio wa Serikali, Wakufunzi, Wathibiti Ubora wa Shule na Maafisa Elimu kwa ushauri wao na kuweza kufanikisha kuandaa mwongozo wa ziara ya nyumbani kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum. Ni matumaini yangu kuwa, shauku kubwa na moyo wa kujituma ulioonekana wakati wa mchakato wa uandaaji wa mwongozo huu utadhihirika wakati wote wa utekelezaji kwa lengo la kupata matokeo chanya, katika kuhakikisha kila mtoto wa kitanzania anapata elimu bora, kwa kuzingatia usawa.

..............................................

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa

**KAMISHNA WA ELIMU**

# DIBAJI

Ufanisi katika utoaji wa elimu bora kwa kuzingatia usawa katika ngazi yoyote ile ya elimu hutegemea ushirikishwaji wa wadau wakiwemo wazazi/walezi, jamii, wanafunzi na walimu kwa kujenga uhusiano mwema katika kutatua changamoto kulingana na mahitaji maalumu ya kielimu kwa kila mwanafunzi. Hivyo, Ziara ya Nyumbani kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum ni njia mojawapo ambayo inakusudia kupunguza changamoto/vikwazo vya ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu ili waweze kupata elimu yenye viwango bora hivyo kutimiza malengo yaliyokusudiwa.

Mwongozo wa Ziara ya Nyumbani kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum unaelekeza jinsi ya kuratibu, kusimamia, kutekeleza, kufuatilia na kutathmini kwa lengo la kutoa maelekezo yatakayowezesha uboreshaji wa Ziara za Nyumbani kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum. Kwa kuzingatia maelekezo yaliyoko katika mwongozo huu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inaamini kwamba, Ziara za Nyumbanikwa wanafunzi wenye mahitaji maalum zitafanyika katika ubora uliokusudiwa ili kuleta matokeo chanya. Shule zote za Msingi na Sekondari zenye wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu (za Serikali na zisizo za Serikali) zinaelekezwa kuzingatia mwongozo huu katika kuratibu, kuendesha, kusimamia, kutekeleza, kufuatilia na kutathmini Ziara za Nyumbani kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum ili kuwepo na viwango vinavyotarajiwa vya

kitaaluma na kitaalamu katika ngazi husika. Kwa kufanya hivyo, wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu nchini watapata fursa na haki ya elimu bora kwa wote bila kubaguliwa na kuweza kutimiza malengo yaliyokusudiwa ya kielimu.

..............................................

Prof. Carolyne I. Nombo

**KATIBU MKUU**

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

# SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

### 1.0 Usuli

Taifa linatambua umuhimu wa utoaji wa Elimu bora kwa kuzingatia usawa na haki kwa watoto wote wakiwemo watoto wenye mahitaji maalum. Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknoloja inatekeleza mikataba, matamko, sera na sheria mbalimbali za kimataifa zinazolenga utoaji wa haki ya Elimu kwa wote bila kubagua kwa misingi ya rangi, dini, jinsi, tofauti za kiuchiumi na kijamii au Ulemavu. Lengo hili limeakisiwa katika Tamko la Dunia Kuhusu Haki za Binadamu la Mwaka 1948, Mkataba wa Kimataifa kuhusu Haki za Mtoto wa Mwaka 1989, Tamko la Elimu kwa Wote la mwaka 1990; Kanuni za Kukuza Usawa wa Fursa kwa watu wenye ulemavu ya Mwaka 1993, Tamko la Kimataifa kuhusu haki ya elimu kwa watu wenye mahitaji maalumu la Mwaka 1994, Mkataba wa Kimataifa kuhusu Ulinzi na Haki za Watu Wenye Ulemavu la Mwaka 2006 na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Kimataifa ya Mwaka 2030. Aidha, Tanzania imesaini na kuridhia mikataba, matamko, Sera na Sheria za Kimataifa iliyoanishwa kwa lengo la kuimarisha mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na ushirikiano wa wazazi na walimu katika kuhakikisha kuwa watoto wote wakiwemo wenye Mahitaji Maalumu wanapata fursa na haki ya elimu bora kwa kuzingatia mahitaji yao katika ujifunzaji.

Sera ya Elimu ya Mwaka 2014, inaelekeza wadau kushiriki kikamilifu katika kuondoa vikwazo vya ujifunzaji

kwa wanafunzi wote wakiwemo wenye Mahitaji Maalumu. Aidha, Mkakati wa Taifa wa Elimu Jumuishi wa Mwaka 2018/2021 unasisitiza umuhimu wa wazazi na walimu kushirikiana katika kuhakikisha kuwa, wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu wanashiriki kujifunza kwa ufanisi na kufikia malengo ya kielimu yaliyopangwa. Vilevile, serikali inatekeleza Sera, Sheria, Mipango, Mikakati na Miongozo mbalimbali ikiwemo Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu wenye Ulemavu ya Mwaka **2004**, Sera ya Maendeleo ya Mtoto Tanzania ya mwaka **2009**, Sheria ya Watu wenye Ulemavu ya Mwaka **2010,** Sheria ya Mtoto ya Mwaka **2010,** Sekta ya Elimu ya Mwaka **2016/2017-2020/2021,** Mpango wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu Awamu ya Kwanza wa Mwaka **2014/2015 - 2018/2019** na mpango wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu Awamu ya Pili wa Mwaka **2019/2020-2022/2023.** Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka **2025.** Juhudi hizo zinalenga kuboresha mazingara ya utoaji wa elimu kwa wanafunzi wote wakiwemo wenye mahitaji maalumu. Vilevile, serikali imeendelea kuanzisha na kuimarisha Umoja wa Wazazi na Walimu (UWAWA) kwa lengo la kujenga uhusiano bora baina ya wazazi/walezi na walimu katika kuwawezesha wanafunzi wote wakiwemo wenye Mahitaji Maalumu kupata elimu bora.

Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum imekuwa ikifanyika kwa nyakati mbalimbali kwa kuzingatia mitazamo ya kidini, kitabibu na kijamii. Katika mtazamo wa kidini iliaminika kuwa, familia yenye mtu mwenye ulemavu ilikuwa na laana, mkosi, au ilifanya dhambi, kwa hiyo Ziara ya Nyumbani wakati huo ilisisitiza familia hiyo kutubu na kuacha dhambi. Aidha, wakati wa mtazamo wa kitabibu

ilisadikika kuwa, watu wenye ulemavu ni wagonjwa na msisitizo uliwekwa kwenye matibabu. Katika mtazamo wa kijamii, msisitizo mkubwa unawekwa katika kumuondolea mtu mwenye ulemavu vikwazo mbalimbali kama vile vikwazo vya kisera, kitaasisi, kimtazamo, kimazingira na kuimarisha ushirikiano kati ya wazazi/walezi na walimu katika utoaji wa huduma za kielimu. Ziara za Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum kimsingi zinafanywa ili kujenga uelewa kwa jamii kuwa watu wenye ulemavu wakiondolewa vikwazo wanaweza kushiriki vizuri katika shughuli za kielimu na hivyo kuchangia katika uchumi wa Taifa. Mtazamo wa kijamii ndiyo unaoendelea kuzingatiwa katika Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum hadi sasa katika nchi yetu.

Utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu katika shule maalumu na vitengo, na shule jumuishi umekuwa ukikabiliwa na vikwazo mbalimbali vikiwemo utoro, mdondoko, kuongezeka kwa kiwango cha kukariri darasa, kutoendelea na ngazi nyingine ya elimu, mimba za utotoni, ndoa za mapema, vitendo vya kikatili na mitazamo hasi kuhusu ulemavu. (MoEST, 2019, 2016 & BEST, 2019). Pamoja na uwepo wa vikwazo, kumekuwepo na jitihada mbalimbali katika kupunguza vikwazo vya utoaji wa elimu ikiwemo Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum. Hata hivyo, ziara hizi zinafanyika bila uwepo wa Mwongozo. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imeona umuhimu wa kuandaa Mwongozo wa Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum ili kuweka utaratibu utakaosaidia katika utekelezaji wa Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum

## 1.1 Muundo wa Mwongozo

Mwongozo huu umegawanyika katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza inatoa taarifa za awali ikiwa ni pamoja na usuli, lengo kuu la Mwongozo, muundo wa Mwongozo, walengwa/wanufaika wa Mwongozo, madhumuni na matokeo tarajiwa ya Mwongozo. Sehemu ya pili inahusu maudhui ya Mwongozo ambayo yamegawanyika katika sura nne: Sura ya kwanza inaeleza dhana ya ziara ya nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum na umuhimu ya Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum.

Katika sura ya pili: Mwongozo unafafanua mambo ya msingi ya kuzingatia kabla, wakati na baada ya Ziara ya Nyumbani. Sura ya tatu: inaelekeza majukumu ya wadau mbalimbali katika kuratibu, kutekeleza, kufuatilia na kutathmini Ziara ya Nyumbani. Sura ya nne: inabainisha suala la kufuatilia na kutathmini Ziara ya Nyumbani.

## 1.2 Malengo ya Mwongozo

Malengo ya mwongozo huu yamegawanyika katika sehemu kuu mbili ambazo ni lengo kuu na malengo mahususi.

### 1.2.1 Lengo kuu la Mwongozo wa Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum

Lengo kuu la Mwongo huu ni Kuweka taratibu za uendeshaji, usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Ziara ya Nyumbani kwa wanafunzi Wenye Mahitaji Maalumu.

### 1.2.2 Malengo Mahususi ya Mwongozo wa Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum.

i. Kuratibu utekelezaji wa Ziara za Nyumbani kwa Wanafunzi Wenye Mahitaji Maalum;

ii. Kubainisha majukumu ya wadau katika utekelezaji wa Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji;

iii. Kufuatilia na kutathimini utekelezaji wa Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum;

iv. Kubainisha wanufaika wa Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum; na

v. Kuanisha mambo ya kuzingatia katika utekelezaji wa Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum.

## 1.3. Walengwa wa Mwongozo

Walengwa wa mwongozo huu ni Wizara yenye dhamana ya Elimu pamoja na Wizara zinazosimamia na kutekeleza utoaji wa Elimu nchini, Halmashauri za Wilaya/Miji/ Manispaa/Majiji, taasisi zinazojihusisha na Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum. Mwongozo huu pia utatumiwa na asasi zisizo za Kiserekali, taasisi za Kiserikali, watu 1.binafsi pamoja na wadau wengine wanaojishughulisha na Ziara ya Nyumbani kwa wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu.

## 1.4 Wanufaika wa Mwongozo

Mwongozo huu unatarajiwa kunufanisha makundi yafuatayo:-

i. Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu wanaosoma shule za Msingi za kutwa zenye Vitengo, Shule Maalumu na Jumuishi;

ii. Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu walioacha shule kwa sababu mbalimbali;

iii. Wanafunzi wanaotarajiwa kuandikishwa shule;

iv. Wanafunzi waliomaliza shule na kufaulu kabla ya kujiunga na ngazi nyingine; na

v. Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu wenye mahudhurio hafifu.

## 1.5 Watumiaji wa Mwongozo

Mwongo unatarajiwa kutumiwa na:-

i. Walimu wanaofundisha wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu wa shule za Msingi za kutwa kwenye Vitengo, shule Maalumu na Jumuishi;

ii. Wathibiti Ubora wa Shule;

iii. Maafisa Elimu;

iv. Walimu wakuu; na

v. Viongozi wa Serikali za (Kata, Kijiji/Mitaa)

## 1.6 Matokeo Tarajiwa ya Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum

Matokeo tarajiwa ya Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum ni pamoja na :-

**i.** Kuwepo kwa idadi kubwa ya wazazi/ walezi na walimu wanaosaidia na kuhakikisha wanafunzi wenye mahitaji maalum wanapata elimu kulingana na malengo ya Taifa ya kupata Mtanzania aliyeelimika mwenye maarifa, stadi, umahiri, uwezo na mitazo chanya na kuweza kuchangia katika kuongeza pato la Taifa. ;

**ii.** Kuimarika kwa Ushirikino baina ya walimu na wazazi/ walezi katika kuhudumia wanafunzi wenye mahitaji maalumu ;

**iii.** Kuondoa mitazamo hasi kwa wazazi/ walezi na jamii kuhusu wanafunzi wenye ulemavu;

**iv.** Kupunguza vikwazo vya ufundishaji na ujifunzaji kwa wananafunzi wenye mahitaji maalum; na

**v.** Kuboresha mawasiliano baina ya wazazi/walezi na walimu wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

# SURA YA PILI

## DHANA YA ZIARA YA NYUMBANI KWA WANAFUNZI WENYE MAHITAJI MAALUM

### 2.0 Maana ya Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum kwa

Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum ni utaratibu wa mawasiliano ya ana kwa ana baina ya mwalimu na wazazi/walezi ambapo mwalimu hupata fursa ya kuyaelewa mazingira ya nyumbani ya mwanafunzi moja moja na kujadili maendeleo ya kitaaluma, makuzi na malezi, na afya ya mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu kwa lengo kutoa afua stahiki.

### 2.1 Umuhimu wa Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum

Ziara ya Nyumbani ni muhimu kwa manufaa ya Wanafunzi wenye mahitaji maalum kwani walimu pamoja na wadau mbalimbali wa Elimu huweza kufahamu mazingira wanayoishi wanafunzi na kufahamu changamoto wanazokumbana nazo wakiwa katika mazingira ya nyumbani na kuweza kuwapa afua stahiki pale inapobidi na kutoa elimu kwa wazazi jinsi ya kuwahudumia wanapokuwa nyumani na kufuatilia maendeleo yao.

### 2.2 Mambo ya Kuzingatia Kabla ya Ziara

i. Kutayarisha ratiba ya ziara kwa muhula au mwaka na kuwasilisha kwa uongozi wa shule kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji;

ii. Kuandaa malengo ya ziara;

iii. Kutoa taarifa ya ziara kwa mzazi au mlezi ikijumuisha malengo, muda, washiriki siku tatu kabla ya ziara;

iv. Kusoma taarifa za awali kuhusu mwanafunzi na familia yake;

v. Kuandaa taarifa za maendeleo ya mwanafunzi kitaaluma, kimakuzi, malezi na kiafya;

vi. Kuandaa shughuli zitakazofanyika wakati wa ziara kwa kuzingatia Mpango Binafsi wa Kielimu wa Mwanafunzi;

vii. Kutoa taarifa ya ziara kwenye uongozi wa serikali ya mtaa/ kijiji anakoishi mzazi/mlezi wa mwanafunzi; na

viii. Kuvaa mavazi yanayozingatia maadili ya kazi.

## 2.3 Mambo ya Kuzingatia Wakati wa Ziara

i. Kuzingatia ratiba ya ziara;

ii. Kutumia muda usiozidi saa moja na usiopungua dakika 30;

iii. Kuwa mnyumbufu wakati wa majadiliano;

iv. Kuongoza majadiliano kwa kutoa nafasi kwa kila mshiriki na kuheshimu mawazo yao;

v. Kuwasilisha taarifa za maendeleo ya mwanafunzi kitaluma, kiafya, makuzi na malezi kwa kuzingatia maadili ya ualimu;

vi. Kuweka mazingira ya kukuza ushirikiano na mahusiano ili kufanikisha malengo ya ziara;

vii. Kuheshimu utamaduni wa familia;

viii. Kutekeleza shughuli iliyokusudiwa kwa kuzingatia Mpango Binafsi wa Kielimu wa Mwanafunzi kwa shirikiana na mzazi/mlezi;

ix. Kuomba ridhaa ya mzazi/ mlezi ili kuchukua nukuu/ picha/rekodi;

x. Kutoa nafasi kwa mzazi/mlezi kueleza kuhusu mafanikio na changamoto zinazomkabili mwanafunzi; na

xi. Kumwomba mzazi/mlezi kutekeleza ushauri wa kitaalamu uliotolewa ili kutatua changamoto zinazomkabili mwanafunzi.

## 2.4 Mambo ya Kuzingatia Baada ya Ziara

**i.** Kuandaa taarifa ya ziara na kuiwasilisha kwakatika uongozi wa shule;

**ii.** Kutunza taarifa za ziara na kuhakikisha kuwa hazitolewi kwa mtu yoyote asiyehusika; na

**iii.** Kutuma nakala ya taarifa ya ziara kwa familia husika.

# SURA YA TATU

## MAJUKUMU MBALIMBALI YA WADAU KATIKA ZIARA YA NYUMBANI KWA WANAFUNZI WENYE MAHITAJI MAALUM

### 3.0 Wadau wa Elimu wana majukumu yafuatayo

### 3.1 Majukumu ya Watumiaji wa Mwongozo

Katika kuhakikisha kuwa kila mtumiaji anatekeleza majukumu yake kama inavyokusudiwa, Mwongozo umebainisha majukumu ya kila mtumiaji kama ifuatavyo.

#### 3.1.1 Majukumu ya Mwalimu Anayefundisha Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu

i. Kutayarisha ratiba ya Ziara ya Nyumbani;

ii. Kufanya mawasiliano na wazazi/walezi kabla ya ziara;

iii. Kufanya Ziara ya Nyumbani kwa kuzingatia ratiba;

iv. Kufuatilia utekelezaji wa masuala yaliyokubaliwa wakati wa ziara;

v. Kutayarisha na kuwasilisha taarifa ya ziara kwa uongozi wa shule;

vi. Kutunza kumbukumbu za taarifa za ziara; na

vii. Kutatua changamoto zitakazobainika wakati wa ziara.

### 3.1.2 Majukumu ya Mwalimu Mkuu

i. Kutenga bajeti ya nauli ili kufanikisha Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum;

ii. Kusimamia na kutathimini utekelezaji wa ratiba za Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum; na

iii. Kutoa taarifa za Ziara ya Nyumbani za Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum kwenye taarifa ya shule.

### 3.1.3 Majukumu ya Afisa Elimu Kata

i. Kusimamia utekelezaji wa Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum katika Shule za Msingi zenye vitengo, Shule Maalumu na Jumuishi ngazi ya Kata;

ii. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum; na

iii. Kuuunganisha taarifa za Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi Wenye Mahitaji Maalum katika taarifa ya utekelezaji wa shughuli za kielimu ngazi ya kata.

### 3.1.4 Majukumu ya Afisa Elimu Maalumu

i. Kuratibu utekelezaji wa Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum katika shule za Msingi zenye Vitengo, Shule Maalumu na Jumuishi ngazi ya Halmashauri;

ii. Kutunza kumbukumbu za taarifa za ziara;

iii. Kuandaa mapendekezo ya bajeti ya kuwezesha Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum kwa ajili ya walimu;

iv. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum katika ngazi ya Halmashauri;

v. Kuunganisha taarifa ya utekelezaji wa Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum katika ngazi ya Halmashauri; na

vi. Kutafuta ufumbuzi wa changamoto zilizobainika katika Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum.

### 3.1.5 Majukumu ya Afisa Elimu Msingi

i. Kusimamia utekelezaji wa Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum katika Shule za Msingi za kutwa zenye vitengo, Shule Maalumu na Jumuishi ngazi ya Halmashauri; na

ii. Kutenga bajeti ya nauli ili kufanikisha Ziara ya Nyumba kwa walimu ni kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalu.

### 3.1.6 Majukumu Mthibiti Ubora wa Shule wa Halmashauri

i. Kufuatilia na kutoa ushauri kuhusu utelekelezaji wa Ziara ya Nyumbani; na

ii. Kuunganisha taarifa ya utekelezaji za Ziara ya Nyumbani za Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum kwenye taarifa ya jumla ya utoaji wa elimu.

### 3.1.7 Viongozi wa Serikali za Mtaa/Kijiji

i. Kuhakikisha ulinzi na usalama kwa washiriki wa Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum; na

ii. Kujenga mahusiano kati ya wazazi/walezi na walimu wa wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu ili kufanikisha Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum.

# SURA YA NNE

## UFUATILIAJI NA TATHMINI

### 4.0. Utangulizi

### 4.1 Maana

Ufuatiliaji ni mchakato endelevu ambao unaangalia utendaji na mafanikio ya utekelezaji wa mwongozo wa Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum. Pia, unatathmini hatua za ufanisi na tija zilizofikiwa katika utekelezaji wa Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum, kubainisha changamoto na kuchukua hatua stahiki za ufumbuzi kwa wakati. Aidha, ufuatiliaji unahusu ukusanyaji wa takwimu na taarifa za utekelezaji wa Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum. Takwimu zinazokusanywa huandikiwa taarifa na kuwasilishwa kwa wadau katika ngazi mbalimbali.

Tathmini ni utaratibu maalumu wa kupima mafanikio ya matokeo ya malengo yaliyokusudiwa. Tathmini inafanywa kila baada ya ziara, wiki, mwezi na mwishoni mwa mwaka. Tathmini hujikita katika kuchambua hatua zilizofikiwa kufanikisha lengo kuu la Ziara ya Nyumbani kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum  ni kuweka taratibu za uendeshaji, usimamizi, ufuatiaji na tathmini ya utekelezaji wa Ziara ya Nyumbani kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu ili kuondoa vikwazo vya ufundishaji na ujifunzaji.

Ufuatiliaji na Tathimini unapaswa kufanywa na mamlaka mbalimbali kama vile:

i. Walimu Wakuu wa Shule;

ii. Maafisa Elimu Kata;

iii. Maafisa Elimu Elimu Maalumu;

iv. Maafisa Elimu Halmashauri;

v. Wathibiti Ubora wa Shule;

vi. Sekretarieti za Mikoa;

vii. Ofisi ya Rais TAMISEMI; na

viii. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

## 4.2 Mbinu za Ufuatiliaji na Tathmini za Ziara ya Nyumbani

Mbinu mbalimbali za ufuatiliaji ambazo zinaweza kutumika ni pamoja na:

i. Mahojiano;

ii. Majadiliano katika vikundi;

iii. Ushuhudiaji; na

iv. Hojaji.

## REJEA

D. L. Olds, H. Kitzman, M. D. Knudtson, E. Anson, J. A. Smith, and R. Cole, “Effect of home visiting by nurses on maternal and child mortality,” *JAMA Pediatrics*, vol. 168, no. 9, pp. 800–806, 2014.View at: Publisher Site | Google Scholar

I. Švab, A. Kravos, and G. Vidmar, “Factors influencing home visits in Slovenian general practice,” *Family Practice*, vol. 20, no. 1, pp. 58–60, 2003.View at: Publisher Site | Google Scholar

P. Braveman, C. Miller, S. Egerter et al., “Health service use among low-risk newborns after early discharge with and without nurse home visiting,” *The Journal of the American Board of Family Practice*, vol. 9, no. 4, pp. 254–260, 1996.View at: Google Scholar

L. A. Roggman, L. K. Boyce, G. A. Cook, and V. K. Jump, “Inside home visits: a collaborative look at process and quality,” *Early Childhood Research Quarterly*, vol. 16, no. 1, pp. 53–71, 2001.View at: Publisher Site | Google Scholar

Mary Ndani, Margaret Mirugami (2009). *Children in need of special protection*. Longhorn Publisher.

Michel M Ndwamo (1993). *Exceptional children Developmental consequences and Intervention*. Longman Kenya Ltd.

*Rasimu ya Utoaji wa Elimu ya Ushauri na Unasihi kwa Wanafunzi* (2019)-WyEST

UNESCO. (1994). *The salamanca statement and framework for action on special needs education.* World conference on special needs education: Access and Quality. Salamanca, Spain.

UNESCO. (2000). *Dakar framework for action: Education for all.* Meeting Our Collective Commitments. World Forum on Education. Dakar, Senegal, 26–28 April 2000, UNESCO, Paris.

URT. (2017). *National strategy on inclusive education 2021/2022–2025/2026*. Ministry of Education, Science and Technology: Dar es Salaam.